
# Je, watu wanaweza kufuatilia ziliko fedha zao?
## Uwazi kuhusu bajeti Afrika Mashariki



## Utangulizi

Pale taarifa kuhusu mgawo wa fedha za bajeti na matumizi yake zinapokosekana, wananchi huachwa bila vidokezo muhimu kuhusu namna kodi wanazolipa zinavyotumika. Ushiriki wa wananchi katika mchakato wa bajeti kupitia tathmini makini ni kipengele muhimu katika mfumo wowote wa udhibiti wa fedha za umma. Je, hali ikoje kuhusiana na suala hili katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki?

Ili kutathmini hali ya upatikanaji wa taarifa ama uwazi katika mchakato wa bajeti, kwa miaka kadhaa sasa Shirika la International Budget Partnership (IBP) limefanya tafiti juu ya Uwazi wa Bajeti (Open Budget Survey) . Tafiti hizi zinatumia mbinu zenye ubora uliohakikiwa ili kupima viwango vya uwazi katika michakato ya bajeti. Utafiti unaofanywa na IBP kwa sasa ndio pekee ulio huru na unaotoa vipimo linganishi kuhusu michakato ya bajeti za serikali. Kuna maswali yapatayo 123 yanayoulizwa katika dodoso na ambayo yamegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza (lenye maswali 92) linapima uwazi wa bajeti kwa wananchi na kukusanya habari kuhusu upatikanaji wa taarifa za bajeti; iwapo taarifa zinatolewa kwa wakati mwafaka; na upana wa taarifa zinazohusu bajeti kwenye ripoti zinazotolewa.[1] Kundi lingine ni maswali yanayopima ufanisi wa ushiriki wa taasisi zinazosimamia mchakato wa bajeti, vyombo vya kutunga sheria[2] (Mabunge) na Taasisi Kuu za Ukaguzi (Supreme Audit Institutions).[3]

Kwa kutumia takwimu kutoka duru tatu za Taftishi ya Uwazi wa Bajeti (2006, 2008 na 2010), muhtasari huu unawasilisha mambo nane juu ya uwazi wa bajeti katika Afrika Mashariki, inayojumuisha Kenya, Sudan, Uganda, Tanzania na Rwanda (taarifa za Burundi hazipo). Muhtasari unaonesha kuna mwelekeo wa kukuza viwango vya uwazi wa bajeti. Hata hivyo, viwango vya uwazi bado ni vya chini,

---

Uwazi
pata picha kamili

Muhtasari huu umeandaliwa na Uwazi-Twaweza,
iliyopo Hivos Tanzania

Uwazi, S.L.P 38342,
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org

Muhtasari huu ulitolewa kwa lugha ya Kiingereza
Novemba 2010 na kutafsiriwa kwa Kiswahili Aprili 2011

IBP INTERNATIONAL BUDGET PARTNERSHIP
Open Budgets. Transform Lives.

na vyombo vya usimamizi vina udhaifu. Imegundulika pia kuwa serikali zinashindwa kuchapisha na kutoa kwa wananchi nyaraka muhimu za bajeti, na kwamba zile nyaraka zinazochapishwa na kutolewa kwa umma huwa zina taarifa chache na za juujuu tu.

Ni wazi kwamba nchi za Afrika Mashariki zinaweza kukuza zaidi viwango vya uwazi kwenye bajeti zao. Kufanya hivyo si vigumu. Baadhi ya hatua ni rahisi sana, kwa mfano, kutoa kwa wananchi nyaraka za bajeti ambazo tayari zinaandaliwa kwa ajili ya matumizi ya ndani ya serikali au kwa ajili ya wahisani. Njia nyingine, kama vile kuimarisha ufanisi wa taasisi za usimamizi kiutendaji—bunge na taasisi kuu za ukaguzi zinaweza kuwa na changamoto zaidi. Hata hivyo, nchi za ukanda wa Afrika Mashariki zilizofanikiwa zinaweza kutoa mwongozo wa namna ya kufanikisha azma hii kwa nchi nyinginezo.

## 2 Mambo nane kuhusu uwazi wa bajeti Afrika Mashariki

### Jambo la kwanza: Uwazi kuhusu bajeti katika Afrika Mashariki ni mdogo sana


Taftishi ya Uwazi wa Bajeti (Open Budget Survey) hutoa alama za uwazi wa bajeti kwa kufuata muundo wa madaraja, ambapo kuna madaraja matano yenye alama 20 kila moja. Kadiri nchi inavyopata alama ya juu zaidi katika skeli ya 0 hadi 100 ndivyo inavyopanda kwenda kwenye daraja bora zaidi. Kwa kutegemea alama zinazotokana na maswali 92 yanayouliza kuhusu upatikanaji, utolewaji kwa wakati mwafaka na mapana/kiwango cha taarifa kwenye nyaraka za bajeti, nchi inaweza kuwekwa katika madaraja yafuatayo:

a. **Hakuna taarifa zinazotolewa au zinatolewa kiduchu**: alama 0-20
b. **Taarifa kidogo sana zinatolewa**: alama 21-40
c. **Baadhi tu ya taarifa ndiyo zinatolewa**: alama 41-60
d. **Taarifa kiasi kikubwa zinatolewa**: alama 61-80, na
e. **Taarifa za kina/zinazotosheleza zinatolewa**: alama 81-100.

Wastani wa alama kwa nchi zote 94 zilizofanyiwa tathmini mwaka 2010 ni 42, hii ikionesha kuwa nchi zinatoa baadhi tu ya taarifa za bajeti kwa umma. Baadhi ya nchi zinafanya vizuri zaidi: alama za India ni 67 (inatoa kiasi kikubwa cha taarifa muhimu) na Marekani ilipata alama 82 (taarifa zinazotosheleza). Nchi iliyoshika nafasi ya juu kabisa katika faharasa ya uwazi wa bajeti ni Afrika Kusini, ambayo ina alama ya ubora wa juu zaidi, alama 92.

Nchi za ukanda wa Afrika Mashariki ziko nyuma zikilinganishwa na nchi zinazofanya vizuri zaidi. Ziko nyuma pia zikilinganishwa na wastani wa dunia. Katika duru mbili za utafiti, mwaka 2008 na 2010 (miaka ambayo data linganishi zinapatikana kwa nchi zote tano zilizotathminiwa), wastani wa alama ambazo nchi za ukanda wa Afrika Mashariki zilipata ni chini ya 40 (kielezo). Kwa hiyo kutokana na taarifa kidogo za bajeti ambazo hutolewa, haiwezekani kwa wananchi wa Afrika Mashariki kuziwajibisha kikamilifu serikali zao kwa namna zinavyosimamia fedha za umma.

**Kielezo 1: Alama kuonesha uwazi wa bajeti kwa kulinganisha Afrika Mashariki na dunia, mwaka 2008 na 2010**





**Chanzo cha takwimu:** Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, 2008 na 2010.

## Jambo la pili: Viwango vya uwazi wa bajeti vinatofautiana sana

Hali ya uwazi wa bajeti inatofautiana mno kati ya nchi na nchi miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki, huku baadhi zikiwa na alama duni, alama 8 (upatikanaji wa taarifa ni tatizo kubwa sana) na baadhi zikiwa na alama za juu, alama 55 (taarifa baadhi tu ndizo hutolewa), (Kielezo 2). Uganda ikiwa na pointi 55, ilifanikiwa kupata alama za juu zaidi kwenye faharasa ya alama za uwazi wa bajeti miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki. Hii, kwa sehemu, ni kutokana na nchi hiyo kuandaa na kutoa kwa wananchi ripoti zote nane muhimu za bajeti zilizobainishwa na tathmini ya uwazi wa bajeti (tazama Jedwali la 1) zikiwemo ripoti za mapitio ya nusu mwaka, na ripoti za mwisho wa mwaka.

Kutokana na Sudan kupata alama 8 na Rwanda alama 11, Sudan na Rwanda ziko katika daraja la chini kabisa la viwango vya uwazi na hii sio tu kwa Afrika bali ni za chini kabisa katika ngazi ya dunia. Nchi hizi hutoa taarifa kiduchu za bajeti kwa wananchi wake.

**Kielezo 2: Faharasa ya Uwazi wa Bajeti kwa nchi kwa mwaka 2010**




**Chanzo cha takwimu:** Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, 2010.

## Jambo la tatu: Mara nyingi nchi za Afrika Mashariki hushindwa kuwapa wananchi nyaraka za bajeti

Ili wananchi waweze kushiriki vizuri katika mchakato wa bajeti, wanahitaji kupata nyaraka muhimu za bajeti kwa wakati. Taftishi ya Uwazi katika mchakato wa bajeti imeweka bayana nyaraka hizo nane za bajeti (Jedwali la 1) na inaonesha kuwa nchi za Afrika Mashariki zinashindwa kuwapa wananchi kitabu cha mapitio ya nusu mwaka (ni Uganda tu ndiyo hutoa kitabu hiki kwa wananchi), na kwa kitabu cha bajeti ya mwananchi (ni Uganda na Rwanda tu ndizo huandaa na kuwapa wananchi). Tanzania na Sudani ndizo zinazofanya vibaya zaidi kwa kushindwa kuupatia umma walau nyaraka tano (5) kati ya nane (8) muhimu za bajeti. Uganda ni nchi pekee inayoandaa, kuchapisha na kutoa kwa umma nyaraka zote muhimu za bajeti.

**Jedwali la 1: Upatikanaji wa nyaraka nane muhimu za bajeti katika nchi za Afrika Mashariki**

| Nyaraka za bajeti | Uganda | Kenya | Tanzania | Rwanda | Sudani |
|---|---|---|---|---|---|
| Mwongozo wa awali wa bajeti | Unatolewa | Unatolewa | Unaandaliwa lakini hautolewi | Unatolewa | Unaandaliwa lakini hautolewi |
| Rasimu ya bajeti kuu | Inatolewa | Inatolewa | Inatolewa | Inaandaliwa lakini haitolewi | Inaandaliwa lakini haitolewi |
| Bajeti iliyopitishwa | Inatolewa | Inatolewa | Inaandaliwa lakini haitolewi | Inatolewa | Inatolewa |
| Bajeti ya wananchi | Inatolewa | Haiandaliwi | Haiandaliwi | Inatolewa | Haiandaliwi |
| Ripoti za ndani ya mwaka | Zinatolewa | Zinatolewa | Zinatolewa | Zinaandaliwa lakini hazitolewi | Zinaandaliwa lakini hazitolewi |
| Mapitio ya nusu mwaka | Yanatolewa | Yanaandaliwa lakini hayatolewi | Hayaandaliwi | Yanaandaliwa lakini hayatolewi | Yanaandaliwa lakini hayatolewi |
| Ripoti ya mwisho wa mwaka | Inatolewa | Inaandaliwa lakini haitolewi | Haiandaliwi | Inatolewa | Inatolewa |
| Ripoti ya ukaguzi | Inatolewa | Inatolewa | Inatolewa | Inatolewa | Inatolewa |
| Hali ya upatikanaji | **8 kwa 8** | **5 kwa 8** | **3 kwa 8** | **5 kwa 8** | **3 kwa 8** |

**Chanzo cha takwimu:** Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, 2010.


Kinachoonekana dhahiri ni kwamba kuna mifano mingi ambapo nyaraka muhimu zinaandaliwa lakini hazitolewi kwa wananchi. Tanzania, kwa mfano, iliandaa vitabu vya bajeti viliyoidhinishwa lakini tofauti na nchi nyingine za Afrika Mashariki, ilishindwa kuvitoa kwa wananchi. Vivyo hivyo, Rwanda na Sudani ziliandaa rasimu ya bajeti kuu, lakini hazikuzitoa kwa wananchi bali zilikuwa kwa matumizi ya ndani ya serikali tu.

### Jambo la nne: Kuna mwelekeo wa kuwepo uwazi zaidi, lakini baadhi ya nchi zinarudi nyuma

Kati ya mwaka 2008 na 2010 alama za ukanda wa Afrika Mashariki katika faharasa ya uwazi wa bajeti ziliongezeka kutoka 29 hadi 34, ikiashiria mwelekeo wa kukua zaidi kwa viwango vya uwazi katika bajeti. Hata hivyo, kuna tofauti katika hatua zilizopigwa kati ya nchi na nchi. Uganda ilipiga hatua kubwa zaidi katika kuboresha uwazi wa bajeti, alama zake ziliongezeka kutoka 32 hadi 55 kati ya mwaka 2006 na 2010 (Kielezo 3). Vilevile, Rwanda na Sudani ziliweza kuongeza alama zao kutoka viwango vya chini kabisa ambavyo nchi hizi zilipata mwaka 2008.

Hata hivyo, siyo nchi zote zinaonesha kupiga hatua kwenda mbele, Kenya na Tanzania zimerudi nyuma. Alama za Tanzania mwaka 2010 ziko juu kuliko zilivyokuwa mwaka 2008, lakini bado ziko chini ya kiwango kilichofikiwa mwaka 2006. Mwaka 2010 Kenya, ilipata alama (48), ambazo ziko chini kwa kulinganisha na alama 57 ilizopata mwaka 2008.

**Kielezo 3: Maendeleo ya nchi katika kukuza viwango vya uwazi katika michakato ya bajeti zao**




**Chanzo cha takwimu:** Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, 2006, 2008 na 2010.

### Jambo la tano: Taarifa zinazotolewa kwenye nyaraka za bajeti ni kidogo sana

Jedwali la 1 limeonesha kuwa nchi nyingi za Afrika Mashariki (isipokuwa Uganda) hazitoi kwa wananchi nyaraka zote muhimu za bajeti. Jedwali la 2 hapo chini linaonesha viwango vya taarifa zilizopo katika nyaraka ambazo hutolewa kwa umma na kwamba kunahitajika kuongezeka kwa ubora zaidi.

Alama za ukamilifu wa taarifa zinazotolewa katika nyaraka za bajeti hukokotolewa kutokana na baadhi ya maswali yanayopima uwazi, kwa kutumia muundo wa madaraja uliooneshwa hapa chini:

a. **Hakuna taarifa zinazotolewa au zinatolewa kiduchu**: alama 0-20, daraja E
b. **Taarifa kidogo sana zinatolewa**: alama 21-40, daraja D
c. **Baadhi tu ya taarifa zinatolewa**: alama 41-60, daraja C
d. **Taarifa kiasi kikubwa zinatolewa**: alama 61-80, daraja B, na
e. **Taarifa za kina/zinazotosheleza zinatolewa**: alama 81-100, daraja A.

Taftishi ya Uwazi wa Bajeti inaonesha kuwa nchi za Afrika Mashariki zinahitaji kuongeza ubora wa viwango vya taarifa wanazozitoa karibu kwenye nyaraka zote nane wanazoandaa na kuzitoa kwa wananchi. Uganda inatoa taarifa za kina na pana zaidi kuliko nchi nyingine zote za Afrika Mashariki. Lakini hata nchi hii nayo hutoa taarifa kidogo kwenye ripoti zake za mapitio ya nusu mwaka na za mwisho wa mwaka, na hutoa baadhi tu ya taarifa kwenye ripoti zake za katikati ya mwaka na ripoti za ukaguzi.

Miongoni mwa nyaraka nane muhimu za bajeti, Rasimu ya Bajeti Kuu ni kitabu muhimu zaidi cha sera na mipango ya nchi. Rwanda na Sudani zote zimeshindwa kutoa kitabu hiki. Kwa upande mwingine licha ya Uganda, Kenya na Tanzania kuchapisha kitabu hiki, nchi hizi zinatoa tatu ya tano au chini ya hapo ya taarifa zilizobainishwa na Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, Uganda ikiwa na alama 62, Kenya alama 55 na Tanzania alama 56.

**Jedwali la 2: Upana na kina cha taarifa zinazotolewa kwenye vitabu vya bajeti**

| Jina la Nyaraka | Uganda | Kenya | Tanzania | Rwanda | Sudan |
|---|---|---|---|---|---|
| Miongozo ya awali ya bajeti | A | A | E | B | E |
| Rasimu kuu ya bajeti | B | C | C | E | E |
| Bajeti iliyopitishwa | A | B | E | A | B |
| Bajeti ya wananchi | B | E | E | A | E |
| Ripoti za mwaka | C | B | B | E | E |
| Mapitio ya nusu mwaka | D | E | E | E | E |
| Ripoti ya mwisho wa mwaka | D | E | E | D | E* |
| Ripoti ya ukaguzi | C | C | C | D | C |

* Hii ni ripoti pekee iliyotolewa na kupata alama E (taarifa kiduchu). Alama E nyingine zote zinawakilisha ripoti ambazo aidha hazikuandaliwa au ziliandaliwa lakini hazikutolewa.

**Chanzo cha takwimu:** Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, 2010.

### Jambo la sita: Mabunge ya nchi yanajihusisha kidogo sana kwenye mchakato wa bajeti

Imekuwa kama jadi kwa watendaji wa serikali[4] kutawala michakato ya bajeti. Hata hivyo, mchakato wenye ufanisi wa bajeti unahitaji kuwapa wananchi fursa ya kupata nyaraka za bajeti, na vilevile kujenga taasisi madhubuti za usimamizi zenye uwezo wa kutathmini kwa makini mapendekezo ya bajeti na utekelezaji wake. Kuwa na vyombo vya usimamizi vilivyo dhaifu ni kutoa mwanya kwa ubadhirifu, kuvurugwa vipaumbele, na wakati mwingine ni chanzo cha mianya ya rushwa. Vyombo madhubuti vya usimamizi, kwa upande mwingine, vinahitaji rasilimali za kutosha, uhuru na mamlaka ya kutosha kuviwezesha kufanya kazi zao bila kuingiliwa.


Taasisi kuu za usimamizi wa bajeti ni Bunge na Taasisi Kuu ya Ukaguzi. Alama za kupima namna taasisi hizi zinavyojihusisha na usimamizi wa bajeti hukokotolewa na kupangwa katika madaraja kama ifuatavyo:

1. **Dhaifu**: alama kati ya 0-33
2. **Wastani:** alama kati ya 34-66
3. **Madhubuti/bora:** alama kati ya 67-100

Kwa ukanda wa Afrika Mashariki, utafiti umebaini kuwa ushiriki wa bunge katika mchakato wa bajeti sio makini kama ambavyo inatarajiwa. Wastani wa alama ya ufanisi wa ushiriki wa Mabunge kwa ukanda huu wa Afrika ni 39, ni mdogo sana. Mabunge ya Sudani na Tanzania yana udhaifu zaidi katika kutimiza wajibu wao kwenye mchakato wa bajeti yakiwa na alama 19 kwa Sudani na 25 kwa Tanzania.

Sababu za udhaifu huu zinatofautiana, lakini sababu iliyo karibu katika kila nchi ni kuwa Bunge linapewa muda mfupi sana na usiotosheleza kuzipitia kwa makini nyaraka za mapendekezo ya bajeti kabla ya kuidhinishwa; linakuwa halina mamlaka au uhuru wa kutosha kufanya/kushinikiza marekebisho ya mapendekezo ya bajeti kuu (ikiwa ni pamoja na mabadiliko katika bajeti ndani ya kipindi cha utekelezaji wa mwaka wa fedha). Pia, imegundulika kwamba bunge linafanya kazi ndogo sana kuzichunguza kwa makini na kuzijadili ripoti zinazotoka Taasisi Kuu ya Ukaguzi.

**Kielelezo 4: Viwango vya ushiriki wa mabunge kwenye mchakato wa bajeti**




**Chanzo cha takwimu:** Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, 2010.


### Jambo la saba: Ushiriki wa Taasisi za Ukaguzi kwenye mchakato wa bajeti ni dhaifu

Taasisi thabiti ya ukaguzi au Ofisi ya Mkaguzi Mkuu ni kiungo kingine cha usimamizi ambacho kinahitajika katika mchakato wa bajeti. Taasisi hii huchunguza kama mapato yanakusanywa na matumizi yanafanyika kwa namna ambayo inakidhi matakwa ya bajeti iliyopangwa kwa kuzingatia kanuni za usimamizi wa fedha za umma.

Alama za ubora wa utendaji wa taasisi za ukaguzi katika Taftishi ya Uwazi wa Bajeti zinashabihiana na zile za Bunge. Wastani wa ngazi ya dunia ni asilimia 49 ikiashiria ushiriki wa wastani. Nchi za Afrika Mashariki zina wastani wa alama 45, chini kidogo ya wastani wa dunia. Uganda na Sudani zina taasisi za ukaguzi dhaifu zaidi kuliko majirani zao, zikiwa na alama 33 kati ya 100. Kenya (alama 57) na Rwanda (alama 53) kwa upande mwingine zina taasisi madhubuti zaidi za ukaguzi.

Taasisi kukosa uhuru kutoka kwa watendaji wakuu wa serikali, kushindwa kuchagua kutokana na kuingiliwa nini kikaguliwe, uhaba wa rasilimali pamoja na kushindwa kutoa taarifa kwa wakati, kushindwa kuwasilisha matokeo vizuri kwa wananchi, na kushindwa kufuatilia kwa kina matokeo ya ukaguzi ni sababu kuu za alama za chini ambazo nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki zimepata katika faharasa ya uwazi wa bajeti duniani.

**Kielezo 5: Ubora wa ushiriki wa Taasisi Kuu ya Ukaguzi kwenye mchakato wa bajeti**




**Chanzo cha takwimu:** Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, 2010.

## Jambo la nane: Sauti za wananchi zinapuuzwa kwa kiwango kikubwa

Ili kukuza mijadala na ushiriki wa wananchi, Bunge lingeweza kufanya vizuri zaidi kama lingeitisha mikutano ya wazi katika kila hatua ya mchakato wa bajeti. Vivyo hivyo, wananchi wanapaswa kupewa fursa na Taasisi za Ukaguzi ya kushiriki moja kwa moja kwenye hatua ya kutathmini mchakato mzima wa bajeti. Utaratibu kama vile kuwa na "fursa ya mawasiliano kuripoti ubadhirifu mara tu unapogundulika" (fraud hotlines) moja kwa moja kwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu inaweza kutumiwa kutoa nafasi muhimu ya ushirikiano kati yao na wananchi.

Taftishi ya Uwazi wa Bajeti inaonesha kuwa nchi za Afrika Mashariki zina upungufu kwenye suala la ushirikishwaji wa wananchi kwenye mchakato wa bajeti. Hili linaashiriwa na majibu yaliyopatikana kwa maswali yanayouliza namna mabunge yanavyoshirikisha wananchi kujadili bajeti na taratibu zinazotumiwa na taasisi za ukaguzi kuwasiliana na wananchi.

Ni Kenya tu ndiyo ina alama zaidi ya 50 kwenye maswali yanayohusiana na mikutano ya Bunge ya wazi inayojumuisha wananchi kujadili masuala ya bajeti. Uganda ni nchi pekee ambayo Taasisi yake kuu ya Ukaguzi imeanzisha utaratibu wa kupokea malalamiko na mapendekezo kutoka kwa wananchi moja kwa moja.

**Jedwali la 3: Usikilizwaji wa sauti za wananchi kwenye mchakato wa bajeti**

| | Alama katikaTaftishi ya Uwazi wa Bajeti | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Vigezo vinavyotathminiwa** | **Kenya** | **Uganda** | **Rwanda** | **Sudani** | **Tanzania** |
| Alama kutoka maswali matatu yanayouliza kuhusu utaratibu wa mikutano ya wazi kwa wananchi (Bunge) | 89 | 44 | 33 | 33 | 0 |
| Utaratibu wa mawasiliano wa Taasisi za Ukaguzi wa kupokea malalamiko na mapendekezo kutoka kwa wananchi (swali la 119) | 0 | 33 | 0 | 0 | 0 |

**Chanzo cha takwimu:** Taftishi ya Uwazi wa Bajeti, 2010.

## Hitimisho

Taftishi ya Uwazi wa Bajeti inaonesha kwamba kumekuwa na ongezeko la wastani kwenye uwazi wa bajeti katika nchi za ukanda wa Afrika mashariki. Hata hivyo, utafiti pia unaonesha kwamba uwazi wa bajeti kwa ujumla bado ni mdogo. Nyaraka muhimu za bajeti haziandaliwi ama zinaandaliwa lakini hazifikishwi kwa wananchi. Zile nyaraka zinazohusu bajeti zinazotolewa zina taarifa ambazo ni za juu juu tu na hazitoshelezi kuwaarifu wananchi kwa kina kuhusu bajeti.

Sudani na Rwanda zinafanya vibaya zaidi katika alama za uwazi, zikiwa kati ya nchi zinazotoa 'taarifa kiduchu', na zikiangukia katika daraja la chini kabisa katika wastani wa ngazi ya dunia. Uganda, Kenya na Tanzania ziko katika daraja la kati katika ngazi ya dunia, zikitoa'baadhi tu ya taarifa'. Ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika Mashariki, Uganda imepiga hatua kubwa zaidi kuelekea kwenye uwazi wa bajeti ndani ya miaka minne iliyopita. Kufanikiwa kwa Uganda katika kukuza viwango vya uwazi wa bajeti kunatoa ushahidi unaoshawishi kuwa inawezekana kupanua uwazi wa bajeti. Vilevile, kuwepo kwa Afrika Kusini katika nafasi ya juu kabisa kwenye chati ya uwazi wa bajeti katika ngazi ya dunia inaonesha kwamba si lazima nchi iwe katika kundi la nchi za OECD[5] ndipo ifanikiwe kufanya vizuri katika kuweka wazi bajeti yake kwa wananchi.

Tofauti ya viwango vya uwazi kati ya nchi mbalimbali za Afrika Mashariki inaashiria uwepo wa fursa kwa kila nchi katika ukanda huu kujifunza kutoka kwa mwenzake. Nchi zenye shauku ya kuendelea haraka zinaweza kuiga hatua zilizochukuliwa na Uganda katika kufanikisha uwazi zaidi kuhusu bajeti. Uganda na nchi nyingine zina mengi ya kujifunza hasa kutoka Kenya na Rwanda kuhusu namna ya kuimarisha ushiriki wa Bunge na Taasisi Kuu ya Ukaguzi kwenye mchakato wa bajeti.

Baadhi ya hatua zinaweza kutekelezwa mara moja. Kwa mfano, kuchapisha nyaraka/vitabu vya bajeti ambavyo tayari vinaandaliwa na kuanzisha utaratibu maalumu wa mawasiliano unaomuwezesha mwananchi kutoa taarifa kwa Mkaguzi Mkuu kuhusu ubadhirifu unaofanyika (fraud hotlines). Pamoja na hayo, nchi zinapaswa kuchukua hatua mbalimbali ili:

- Kuongeza ubora wa upana wa taarifa zinazotolewa kwenye nyaraka za bajeti;
- Kuimarisha taasisi za usimamizi kwa kuziongezea rasilimali, mamlaka na uhuru wa kufanya kazi zao bila kuingiliwa; na
- Kutoa fursa ya mikutano ya wazi ya kujadili bajeti ili wananchi waweze kushirikiana moja kwa moja na Bunge kwenye mchakato wa bajeti.

Serikali hutumia fedha za umma kwa niaba ya wananchi, na wananchi wana haki ya kufuatilia namna fedha zao zinavyotumika. Uwazi zaidi kwa wananchi unaweza kukuza uwajibikaji na ufanisi, na kuimarisha uhalali wa serikali kwenye macho ya umma.

## Rejea

IBP (2006, 2008 na 2010), The Open Budget Index. Ilichukuliwa tarehe 21 Oktoba, 2010 kutoka http://www.internationalbudget.org/what-we-do/open-budget-survey/?fa=full-report.

# Kiambatisho: Faharasa ya Uwazi wa Bajeti, 2010

| Jina la nchi | Alama | Madaraja ya uwazi wa bajeti |
|---|---|---|
| Afrika Kusini | 92 | Hutoa taarifa za kutosheleza |
| New Zealand | 90 | |
| Uingereza | 87 | |
| Ufaransa | 87 | |
| Norway | 83 | |
| Sweden | 83 | |
| Marekani | 82 | |
| Chile | 72 | Hutoa taarifa za kiwango kikubwa |
| Brazili | 71 | |
| Korea Kusini | 71 | |
| Slovenia | 70 | |
| Ujerumani | 68 | |
| Sri Lanka | 67 | |
| India | 67 | |
| Peru | 65 | |
| Polandi | 64 | |
| Hispania | 63 | |
| Jamhuri ya Czech | 62 | |
| Ukraine | 62 | |
| Kolumbia | 61 | |
| Urusi | 60 | Hutoa baadhi ya taarifa |
| Mongolia | 60 | |
| Romania | 59 | |
| Italia | 58 | |
| Ureno | 58 | |
| Papua New Guinea | 57 | |
| Croatia | 57 | |
| Slovakia | 57 | |
| Uturuki | 57 | |
| Ajentina | 56 | |
| Bulgaria | 56 | |
| Uganda | 55 | |
| Ufilipino | 55 | |
| Georgia | 55 | |
| Ghana | 54 | |
| Serbia | 54 | |
| Namibia | 53 | |
| Mexico | 52 | |
| Botswana | 51 | |
| Indonesia | 51 | |
| Jordan | 50 | |
| Guatemala | 50 | |
| Kenya | 49 | |
| Misri | 49 | |
| Macedonia | 49 | |
| Bangladesh | 48 | |
| Malawi | 47 | |
| Costa Rica | 47 | |
| Nepal | 45 | Hutoa baadhi ya taarifa |
| Tanzania | 45 | |
| Bosnia-Herzegovina | 44 | |
| Azerbaijan | 43 | |
| Thailand | 42 | |
| Liberia | 40 | Hutoa taarifa kidogo |
| Malaysia | 39 | |
| Pakistani | 38 | |
| Kazakhstani | 38 | |
| El Salvador | 37 | |
| Nikaragua | 37 | |
| Zambia | 36 | |
| Mali | 35 | |
| Timor-Leste | 34 | |
| Venezuela | 34 | |
| Albania | 33 | |
| Trinidad and Tobago | 33 | |
| Lebanoni | 32 | |
| Ecuador | 31 | |
| Msumbiji | 28 | |
| Morocco | 28 | |
| Angola | 26 | |
| Yemeni | 25 | |
| Afghanistani | 21 | |
| Nigeria | 18 | Hutoa taarifa chache sana au hakuna |
| Jamhuri ya Kyrgyz | 15 | |
| Kambodia | 15 | |
| Jamhuri ya Dominika | 14 | |
| Vietnam | 14 | |
| Bolivia | 13 | |
| China | 13 | |
| Honduras | 11 | |
| Rwanda | 11 | |
| Sudan | 8 | |
| Jamhuri ya | 6 | |
| Kidemokrasia ya Kongo | 5 | |
| Burkina Faso | 3 | |
| Niger | 3 | |
| Senegali | 2 | |
| Kameruni | 1 | |
| Saudi Arabia | 1 | |
| Algeria | 0 | |
| Chadi | 0 | |
| Iraki | 0 | |
| Equatorial Guinea | 0 | |
| Fiji | 0 | |
| São Tomé Príncipe | | |

## Vidokezo

**1 OBS inaangalia uwazi juu ya nyaraka muhimu zifuatazo:**

**Mwongozo wa awali wa bajeti:** Waraka huu unaweka vigezo vya awali ambavyo vinaelekeza jinsi bajeti inayofuata ya serikali itakavyokuwa.

**Rasimu ya bajeti kuu:** kitabu muhimu zaidi cha kisera cha serikali. Kinawasilisha namna ambavyo serikali inapanga kukusanya mapato na maeneo fedha zilikopangiwa kutumika, hivyo kuyaweka malengo ya sera kwenye vitendo.

**Bajeti iliyopitishwa:** ambayo huwa sheria ya nchi na hutoa taarifa za msingi kwa ajili ya uchambuzi wote wa bajeti unaofanywa kipindi cha mwaka wa fedha. Kwa ujumla, bajeti iliyopitishwa inapaswa kuwapatia wananchi takwimu na taarifa ambazo wanaweza kuzitumia kutathmini vipaumbele vya sera za serikali vilivyoelezwa na kuiwajibisha serikali.

**Bajeti ya wananchi:** ni kijitabu kinachowasilisha kwa njia rahisi bajeti ya serikali chenye madhumuni ya kuuwezesha umma/wananchi — wakiwemo wale wasiojua masuala ya fedha za umma — kuelewa mipango ya serikali.

**Ripoti za ndani ya mwaka:** Hizi zinatoa picha ya awali ya namna bajeti inavyotekelezwa katika kipindi cha mwaka wa bajeti. Zinaruhusu ulinganishaji na tarakimu za bajeti iliyopitishwa na hivyo kuwezesha ufanyikaji wa marekebisho.

**Mapitio ya nusu mwaka:** hutoa picha ya kina kwa jumla ya matokeo ya utekelezaji wa bajeti katikati ya mwaka wa fedha na inajadili mabadiliko yoyote yaliyojitokeza katika nyanja za kiuchumi ambayo yanaathiri sera za bajeti zilizopitishwa. Taarifa hizi zinatoa fursa kwa serikali, Bunge na umma kubaini iwapo kuna haja ya kufanya marekebisho yoyote kuhusiana na mapato, matumizi au mikopo kwa kipindi kilichobakia cha mwaka wa utekelezaji wa bajeti.

**Ripoti ya mwisho wa mwaka:** hii inalinganisha utekelezaji halisi wa bajeti na bajeti iliyopitishwa. Ripoti ya mwisho wa mwaka inawataarifu watunga sera juu ya sera za kodi, mahitaji ya mikopo, na vipaumbele vikuu vya matumizi, hivyo inaharakisha marekebisho kwa miaka ijayo ya bajeti.

**Ripoti ya ukaguzi:** Hii ni tathmini ya hesabu za serikali inayofanywa na Taasisi Kuu ya Ukaguzi. Inaarifu iwapo serikali imekusanya mapato na kuyatumia kulingana na mipango na taratibu za bajeti iliyoidhinishwa. Inatoa taarifa iwapo uwekaji kumbukumbu za hesabu za serikali uko sawasawa na umefanywa kwa umakini, na kama kulikuwa na kasoro kwenye usimamizi wa fedha za umma.

**2 Chombo cha kutunga sheria** (Bunge) kinatakiwa kuidhinisha bajeti inayowasilishwa kwake na kinatarajiwa kuiwajibisha serikali kwa utendaji wake katika kutekeleza bajeti.

**3 Taasisi Kuu ya Ukaguzi** inalisaidia Bunge kusimamia bajeti. Taasisi ya ukaguzi inaweza kupatiwa jina lolote kama vile Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu, Bodi ya Ukaguzi, au Mahakama ya Hesabu.

**4 Watendaji wakuu** katika matumizi ya fedha za umma kwa kawaida huwakilisha Wizara ya Fedha au Hazina. Ni taasisi ambayo kimsingi ndiyo yenye wajibu wa kuandaa data za bajeti.

**5 OECD** (Organisation for Economic Cooperation and Development) ni Ushirikiano wa masuala ya kiuchumi na maendeleo wa mataifa yenye kipato cha juu.